MWENGE GOSPEL RUNNERS

# MAPAMBANO

Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."

"Waefeso 6:12.




## MAADUI WANAOTUKABILI KILA SIKU MAISHANI



**ULEVI**

Huvuruga akili, afya na maisha ya milele.



**RUSHWA**

Huchafua mioyo na kuharibu jamii.



**UBINAFSI**

Hufanya tusisijali wengine wala kuwapenda.



**UZINZI**

Huharibu heshima na kuleta mateso.



**CHUKI**

Huvunja mahusiano na kuleta vita.



**NGOJA KIDOGO**

Mtego hatari zaidi unaokupoteza milele!

## BADO KUNA NAFASI YA KUJIPONYA

Mungu anakupenda sana tazama upande wa nyuma utaona njia ya kuelekea tumaini jipya maishani.

# KWANINI WATU WENGI HAWATAKI KUMWAMINI YESU?



Shetani amewatia Upofu wasiweze kuona tumaini.

*"ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu." 2 Wakorintho 4:4.*

## NJIA YA TUMAINI - HATUA 4 ZA KUMJUA MUNGU

### 1 TAMBUA



Kubali kwamba wewe ni mwenye dhambi.

(Warumi 3:23)

### 2 AMINI



Amini kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zako na kufufuka.

(Yohana 3:16)

### 3 TUBU



Tubu dhambi zako na umwombe Mungu akusamehe.

(1 Yohana 1:9-10)
(Matendo 3:19)

### 4 MPOKEE



Mpokee Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wako.

(Warumi 10:9-10)

## TAMKA SALAHII KUANZA MAISHA MAPYA

Mungu Baba katika jina la Yesu Kristo, nakuja mbelezako kwa shukrani, nikitambua upendo wako kwangukwa kumtoa mwanao wa pekee, ili afanyike dhabihu yadhambi zangu na kuondoa lile pazia lililonitenga nawe.Ninatubu dhambi zangu zote na kumpinga shetani katikamaisha yangu. Natamka kwa kinywa changu kuwa YesuKristo ni Bwana na mwokozi wa maisha yangu. BwanaYesu, naomba uje ufanye makao ndani yangu pamoja naMungu Baba na Mungu Roho Mtakatifu. Nielekeze kwenye kweli yote na unipe ujasiri wa kuandamana nawe kila sikuza maisha yangu. Asante kwa kunifanya kuwa kiumbekipya, ninaomba na kuamini katika jina la Yesu, Amen.





## UAMUZI NI WAKO
## *AMUA SASA!*








Soma Neno la Mungu kila siku, na omba ili upate kukua kiroho. (2 Timotheo 3:16-17)

Kama ungependa kupata msaada zaidi wa jinsi ya kuanza safari yako na Mungu, Sisi tunapatikana Kanisa la T.A.G Mwenge Christian Centre, Dar es Salaam.

**IDARA YA UINJILISTI**
0713250034